Jina ..... **Nambari yako** .....

Shule ..... Sahihi .....

102 Tarehe .....

KISWAHILI
Oktoba 2016
Muda: Saa 2½

Www.Manyamfranchise.Com

KIDATO CHA PILI

KISWAHILI
Oktoba 2016
Muda: Saa 2½

MAAGIZO

a) Jibu maswali yote.
b) Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

Swali	Alama	Tuzo
1. Insha	20	
2. Ufahamu	20	
3. Sarufi na Matumizi ya Lugha	40	
4. Isimujamii	10	
5. Fasihi Simulizi	10	

INSHA

Maagizo

1. *Insha yako isipungue maneno 400*
2. *Insha hii ina alama 20*
3. *Lazima insha hii iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

Andika mahojiano baina ya askari na mshukiwa wa wizi.

Www.Manyamfranchise.Com

Www.Manyamfranchise.Com

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma.

Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila moja wapo ina athari zake. Kwa mfano kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serkali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki shamba, vitambulisho n.k. kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kama ugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya. Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini.

Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyikazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule, hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma na kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, mahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa majukumu yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalam huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo ili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale wasiojimudu kifedha hubaki wakilia ngao. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuaanza kuhudumia jamii.

Ufisadi umekita mizizi na kushamiri katika sekta za kibinasfi kwa upande wa kuajiri wafanyikazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo na kuajiri wafanyikazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo. Kwa hivyo wafanyikazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha pale pale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimeteuliwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza kashfa ya 'Goldenberg' ambapo pesa za umma (mabilioni ya shilingi) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia zisizo halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahijajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malamiko kutoka kwa wananchi waliohasiriwa na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa wakalipa, au wakilipwa kuwatetea mahakamani wanakepwa jukumu hila ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

a) Kwa nini mwandishi anauona ufisadi kama uhalifu. (alama 1)

.....

.....

b) Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu. (alama 4)

.....

.....

www.Manyamfranchise.com

.....

.....

c) Kulingana na kifungu ulichosoma. Ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

d) Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

e) Kwa nini mwandishi anasema kwamba ufisadi umekita mizizi na kushamiri. (alama 3)

.....

.....

.....

f) Toa sababu mbili kuonyesha kuwa mwandishi ana matumaini kuwa ufisadi utaangamizwa. (alama 2)

.....

.....

.....

g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

i) Majukumu

.....

ii) Wakilia ngoa

.....

iii) Waliohasiriwa

.....

www.Manyamfranchise.Com

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Taja sauti nne zinazojulikana kama nazali. (alama 2)

.....

.....

.....

.....

b) Onyesha kikundi nomino na kikundi tenzi katika sentensi hii.
Mama aliyekuwa akipiga kelele ameenda kulala (alama 2)

.....

.....

c) Tambulisha viambishi awali na viambishi tamati katika neno hili. (alama 2)
Watakaohukumiwa

.....

.....

d) Yaweke maneno haya katika ngeli zake. (alama 2)

i) Mejeruhi .....

ii) Ofisi .....

e) Andika nomino zifuatazo katika udogo na ukubwa. (alama 2)

	Udogo	Ukubwa
i) Kiatu	.....	.....
ii) Mdudu	.....	.....

f) Bainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Ameweza kusoma vitabu vingi kwani vimenunuliwa.

.....

.....

g) Kamilisha jedwali lifuatalo. (alama 2)

Kitenzi	Kutendeana	Kutendesha
i) Inua		
ii) Paa		

h) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo :
Nyanya yangu aliinama aliponiona. (alama 2)

.....

i) Kanusha sentensi hii: (alama 2)
Wamekuwa wakilala darasani tangu asubuhi.

.....

www.Manyamfranchise.Com

j) Unda nomino mbili mbili kutokana na maneno yafuatayo. (alama 2)

i) lea

.....

.....

ii) ruka

.....

.....

k) Tunga sentensi moja pekee ukidhihirisha maana tofauti za maneno yafuatayo. (alama 2)
i) Doa

.....

ii) Ndoa

.....

l) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 2)
Kitabu kinachopendwa ni kile kinachopendeza.

.....

m) Andika kwa wingi: (alama 2)
Jalala lake lina vitabu viwili

.....

n) Onyesha na ueleze aina za nomino katiak sentensi hii. (alama 2)
Juma alihusika katika wizi jana usiku.

.....

.....

o) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (alaam 3)
"Kesho mtafanya mtihani wa Kiswahili," mwalimu alitueleza.

.....

.....

p) Eleza matumizi ya vitawe vilivyopigiwa mstari katika sentensi hii. (alama 2)
i) <u>Haya</u> unayoyafanya yatakutia <u>haya</u>.

.....

q) Weka shadda katika maneno yafuatayo: (alama 2)

i) Kitabu .....

ii) Mto .....

r) Taja vipashio vya lugha. (alama 2)

.....

.....

www.Manyamfranchise.Com

s) Yakinisha sentensi ifuatayo.
Asingesoma kwa bidii asingepita mtihani huo. (alama 2)

.....

.....

4. ISIMUJAMII

a) Eleza kaida tano za lugha. (alama 5)

.....

.....

.....

.....

.....

b) Eleza sifa tano za sajili ya hotelini. (alama 5)

.....

.....

.....

.....

.....

5. FASIHI SIMULIZI (ALAMA 10)

a) Kwa kutumia hoja nne onyesha umuhimu wa nyimbo katika jamii. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

b) Taja na ueleze aina tatu za hadithi. (alama 6)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

www.Manyamfranchise.Com